

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DIVISHENI YA KAZI
ILİYOKETI DAR ES SALAAM.
MAOMBI ANUAI NAMBA. 376 YA 2022

*(Maombi haya yanatokana na maombi ya Ukaziaji Deni Tuzo Na. 343 ya 2022
yalipo mbele ya Mahakama Kuu-Divisheni ya kazi)*

SHOMARY SHOMARY SALUM.....MLETA MAOMBI

DHIDI YA

KHALSA SPORTS CLUB

(PUNJAB RASOI RESTAURENT)MJIBU MAOMBI

UAMUZI MDOGO

K. T. R. Mteule, J.

09 Machi 2023 & 16 Machi 2023

Maamuzi haya yanatokana na maombi ya mwombaji ambaye anaomba Mahakama impe kibali cha kuunganishwa kama mmoja wa washindi wa deni tuzo katika Mgogoro wa Kikazi Na. CMA/DSM/ILA/96/19/62. Mwombaji anaiomba Mahakama hii kutoa nafuu zifuatazo;-

- i) Kwamba, Mahakama hii itoe kibali cha kumruhusu na kuunganishwa na kuwa mmoja wa washinda tuzo kama msimamizi wa mirathi ya marehemu SHOMARI SALUM KIDUNDA kwenye shauri la utekelezaji lililotokana na mgogoro wa Kikazi Na. CMA/DSM/ILA/96/19/62

ii) Na amri nyinginezo ambazo Mahakama hii tukufu itaona zinastahili.

Maombi haya yameambatana na kiapo cha Bw. Shomary Shomary Salum ambaye ndiye mleta maombi. Mjibu Maombi hakuweza kuleta pingamizi kwa mujibu wa Kanuni ya 24 (4) ya Kanuni za Mahakama ya Kazi kwa kuwa hakufika Mahakamani. Maombi yalisikilizwa upande mmoja baada ya Mahakama kujiridhisha kwamba mjibu maombi alipokea kuitwa shaurini bila kufika. Shauri hili liliendeshwa kwa njia ya mdomo na Mleta Maombi aliwasilishwa na Bw. Kelvin Mundo ambaye ni Muwakilishi Binafsi.

Katika mawasilisho yake, Bw. Mundo alieleza kwamba mleta maombi anaomba Mahakama hii itoe kibali cha kuunganishwa kama mmoja wa washinda Tuzo katika mgogoro wa kazi Na. CMA/DSM/ILA/96/19/62. Alieleza anaomba kuunganishwa kwa ajili ya kusimamia mirathi ya marehemu Shomary Salum Kidunda. Aliendelea kueleza ya kwamba Mleta maombi alifungua **Maombi Na. 556 ya 2022** katika Mahakama ya mwanzo Temeke ambapo aliteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ya marehemu Shomary Salum Kidunda ambaye ndiye mshindi wa deni Tuzo dhidi ya Khalsa Sports Club (Punjab Rasoi Restaurant) ambaye ndiye aliyekuwa muajiri wa Marehemu.

Baada ya kuzingatia maelezo ya mleta maombi, Mahakama inaona kuwa hoja iliyopo mbele yake ni endapo mwombaji ni mtu muhimu anayestahili kuunganishwa kuwa mmoja wa washindi wa deni tuzo?

Hakuna ubishi ya kwamba mshindi wa deni Tuzo katika mgogoro wa Kikazi Na. CMA/DSM/KIN/R.900/2017 alifariki, na kwamba mleta maombi aliteuliwa kama msimamizi wa mirathi. Kama kuna maombi ya utekelezaji wa deni tuzo, mahakama hii inaona umuhimu wa kuhusika msimamizi wa mirathi katika maombi hayo ili kutoathiri zoezi la ukaziaji Hukumu. Hata hivyo haitakuwa sawa mleta maombi aongezwe kama mshindi wa tuzo, bali anaweza kuwekwa kama msimamizi wa mirathi ya mshindi wa tuzo.

Hivyo maombi haya yanaruhusiwa kwa kiwango cha mleta maombi kuongezwa katika maombi ya deni Tuzo kama msimamizi wa mirathi ya mshinda Tuzo Bw. Shomari Marehemu Kidunda na siyo kama mmoja wa washinda tuzo. Imeamriwa hivyo.

Imetolewa Dar es Salaam leo tarehe 16 Machi, 2023.



KATARINA REVOCATI MTEULE

JAJI

16/03/2023

